TANGAZO LA SERIKALI NA. 04 la tarehe 9/1/2026

SHERIA YA TAFSIRI YA SHERIA,
(SURA YA 1)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 85(4))*

NOTISI YA TOLEO RASMI LA TAFSIRI YA SHERIA KUU ZILIZOTAFSIRIWA KWA LUGHA YA KIINGEREZA YA MWAKA 2026

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Toleo Rasmi la Tafsiri ya Sheria Kuu zilizotafsiriwa kwa Lugha ya Kiingereza ya mwaka 2026.

Sheria zilizotafsiriwa

**2**.-(1) Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi, Sura ya 38 na Sheria ya Bima Afya kwa Wote, Sura ya 161 zimetafsiriwa kutoka lugha ya Kiswahili ambayo ilitumika wakati wa kutungwa kwenda katika lugha ya Kiingereza na zinatangazwa kuwa ni Toleo Rasmi la Tafsiri ya Sheria hizo.

(2) Sheria zilizotafsiriwa ni sheria zilizojumuishwa katika Toleo la Nyongeza la 2025 la Toleo la Urekebu la Mwaka 2023.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA · OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

Dodoma,
6 Januari, 2026

HAMZA S. JOHARI
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*